TANGAZO LA SERIKALI NA. 856 la tarehe 11/10/2024

SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA,
(SURA YA 290)

KANUNI

(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 37A(4))

KANUNI ZA UTOAJI NA USIMAMIZI WA MIKOPO KWA VIKUNDI VYA WANAWAKE, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU ZA MWAKA 2024

MPANGILIO WA KANUNI

Kanuni *Jina*

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

1. Jina.
2. Matumizi.
3. Tafsiri.

SEHEMU YA PILI
UTENGAJI, UTOAJI NA UREJESHAJI WA MIKOPO

4. Wajibu wa kutenga fedha.
5. Mgao wa fedha za mikopo.
6. Sifa za kupata mkopo.
7. Mkopo kwa mtu mwenye ulemavu.
8. Utaratibu wa uombaji wa mikopo.
9. Utaratibu wa utoaji wa mikopo.
10. Matumizi ya fedha za mikopo.
11. Urejeshaji wa mikopo.
12. Kuchelewesha marejesho ya mikopo.
13. Kushindwa kurejesha mkopo.
14. Nyongeza ya muda wa kurejesha mkopo.

SEHEMU YA TATU
USIMAMIZI WA MIKOPO

15. Majukumu ya Mkurugenzi.
16. Majukumu ya Afisa Maendeleo ya Jamii.
17. Majukumu ya Afisa Biashara.
18. Wajibu wa Mweka Hazina.
19. Wajibu wa Mkaguzi wa Ndani.
20. Kamati ya huduma za mikopo ngazi ya kata.
21. Majukumu ya Kamati ya Huduma ya Mikopo ngazi ya Kata.
22. Kamati ya Huduma ya Mikopo ngazi ya Halmashauri.
23. Majukumu ya Kamati ya Huduma ya Mikopo ngazi ya Halmashauri.
24. Kamati ya Wilaya ya Uhakiki wa Mikopo.
25. Majukumu ya Kamati ya Wilaya ya Uhakiki wa Mikopo.
26. Majukumu ya Timu ya Menejimenti.
27. Majukumu ya Kamati ya Kudumu ya Fedha, Uongozi na Mipango na kamati ya kudumu ya fedha na utawala.
28. Majukumu ya Baraza la Madiwani.
29. Wajibu wa Kamati ya Bajeti ya Halmashauri.
30. Kamati ya uratibu wa Mikopo ngazi ya Mkoa.
31. Majukumu ya kamati ya uratibu wa mikopo ngazi ya mkoa.
32. Kitengo cha uratibu wa utoaji na usimamizi wa mikopo ya vikundi.

SEHEMU YA NNE
UTOAJI WA MIKOPO KWA UTARATIBU WA TAASISI ZA FEDHA

33. Utoaji wa Mikopo kwa utaratibu wa taasisi za fedha.
34. Ufuatiliaji na ukusanyaji wa marejesho.
35. Majukumu ya pande zote.
36. Tathmini na uboreshaji.

SEHEMU YA TANO
MASHARTI YA JUMLA

37. Akaunti Maalum ya Mikopo.
38. Mafunzo na ufuatiliaji wa mikopo ya vikundi.
39. Akaunti Maalum ya Mikopo.
40. Mafunzo na ufuatiliaji wa mikopo ya vikundi.
41. Kuhitimu ukopaji.
42. Makosa na adhabu.
43. Kufutwa kwa Kanuni.

Tangazo la Serikali Na. 856 (Linaendelea)

SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA,
(SURA YA 290)

KANUNI

(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 37A(4))

KANUNI ZA UTOAJI NA USIMAMIZI WA MIKOPO KWA VIKUNDI VYA WANAWAKE, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU ZA MWAKA 2024

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina

1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Utoaji na Usimamizi wa Mikopo kwa Vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu za Mwaka 2024.

Matumizi

2. Kanuni hizi zitatumika katika Mamlaka za Serikali za MitaaTanzania Bara.

Tafsiri

3. Katika Kanuni hizi, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo:

"ajira rasmi" maana yake ni aina ya ajira inayozingatia sheria na taratibu za ajira katika sekta ya umma au sekta binafsi ambapo mfanyakazi huajiriwa kwa mujibu wa mkataba ambao unajumuisha taarifa za mshahara, posho maalumu, saa za kufanya kazi, likizo, haki na wajibu wa mwajiri na mwajiriwa, malipo ya kodi, mchango wa bima ya afya na pensheni;

"Kamati ya Huduma za Mikopo" maana yake ni Kamati ya Huduma za Mikopo iliyoanzishwa chini ya Kanuni hizi;

"Kamati ya Wilaya ya Uhakiki wa Mikopo" maana yake ni Kamati ya Uhakiki wa Mikopo iliyoanzishwa chini ya Kanuni hizi;

"Kamati ya Kudumu ya Fedha, Uongozi na Mipango" maana yake ni Kamati ya Kudumu ya Fedha, Uongozi na Mipango ya Mamlaka ya Wilaya;

"Kamati ya Kudumu ya Fedha na Utawala" maana yake ni Kamati ya Kudumu ya Fedha na Utawala ya Mamlaka za Miji;

"kijana" maana yake ni mtu mwenye umri wa kuanzia miaka 18 hadi 45;

"Mamlaka ya Serikali ya Mitaa" maana yake ni halmashauri ya wilaya, mji, manispaa au jiji;

"mkopo" maana yake ni fedha taslimu, vifaa au fedha pamoja na vifaa vinavyotolewa na mamlaka za serikali za mitaa kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa;

Sura ya 342

"taasisi ya fedha" itakuwa na maana kama ilivyotafsiriwa kwenye Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha; na

"Timu ya Menejimenti" maana yake ni Mkurugenzi na Wakuu wa divisheni na vitengo katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

SEHEMU YA PILI
UTENGAJI, UTOAJI NA UREJESHAJI WA MIKOPO

Wajibu wa kutenga fedha

4.-(1) Mamlaka ya Serikali za Mitaa itakuwa na wajibu wa kutenga asilimia kumi ya mapato yanayokusanywa kutoka kwenye vyanzo vya ndani vya mapato kwa ajili ya kutoa mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

(2) Katika kutekeleza masharti ya kanuni ndogo ya (1), Mkurugenzi akiwa kama Afisa Masuuli atakuwa nawajibu wa kuhakikisha kuwa:

(a) Mamlaka ya Serikali za Mitaa inatenga asilimia kumi ya mapato ya ndani kwa ajili ya kutoa mikopo;

(b) mikopo inatolewa kwa kuzingatia masharti ya Kanuni hizi; na

(c) vikundi vilivyokopeshwa vinarejesha mikopo kwa mujibu wa mkataba.

Mgao wa fedha za mikopo

5.-(1) Mamlaka ya Serikali za Mitaa itatumia fedha zilizotengwa kwa mujibu wa kanuni ya 4 kutoa mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kanuni ndogo ya (1), Mamlaka ya Serikali za Mitaa itatoa mikopo kwa kuzingatia mgawo ufuatao:

(a) asilimia arobaini ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya mikopo ya vikundi vya wanawake;

(b) asilimia arobaini ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya mikopo ya vikundi vya vijana; na

(c) asilimia ishirini ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya mikopo ya vikundi vya watu wenye ulemavu.

(3) Endapo fedha zilizotengwa kwa kundi mojawapo kati ya makundi yaliyoainishwa kwenye Kanuni ndogo ya (2), hazikutumika kutokana na kutokupokea maombi au kuwepo kwa fedha zilizobaki kwenye fungu husika, Mamlaka ya Serikali za Mitaa inaweza kutoa mkopo kwa kundi lingine lililoainishwa katika kifungu hiki kutoka katika asilimia iliyotengwa kwa ajili ya kundi jingine lenye mahitaji zaidi.

(4) Mikopo itakayotolewa chini ya Kanuni hizi haitatozwa riba.

Sifa za kupata mkopo

6.-(1)Bila kuathiri masharti ya Kanuni hizi, kikundi cha wanawake, vijana au watu wenye ulemavu kitakuwa na sifa ya kupatamkopo endapo:

(a) wanakikundi wake ni raia wa Tanzania wenye akili timamu na umri usio chini ya miaka kumi na nane;

(b) kimetambuliwa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa kupitia mfumo wa kieletroniki wa utoaji na usimamizi wa mikopo;

(c) kinajishughulisha na ujasiriamali au kinakusudia kuanzisha shughuli za ujasiriamali mdogo au wa kati;

(d) kwa kikundi cha wanawake au vijana, kina idadi ya wanakikundi wasiopungua watano na kwa kikundi cha watu wenye ulemavu, kina idadi ya wanakikundi wasiopungua wawili;

(e) kina akaunti ya benki iliyofunguliwa kwa jina la kikundi kwa ajili ya matumizi ya

kikundi;

(f) hakina wajumbe wenye ajira rasmi; na

(g) kimepata mafunzo ya ujasiriamali.

(2) Bila kujali masharti ya kanuni ndogo ya (1), kikundi kitahesabika kuwa kimepoteza sifa ya kupata mkopo endapo:-

(a) kitapoteza moja wapo ya sifa zilizoainishwa katika kanuni ndogo ya(1);

(b) hakijamaliza au kimeshindwa kurejesha mkopo uliotolewa chini ya Kanuni hizi;

(c) kimetoa taarifa za uongo kwa Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa lengo la kupata mkopo;

(d) kimetumia fedha za mkopo kwa matumizi tofauti na yale yaliyoombewa mkopo bila ya idhini ya Timu ya Menejimenti.

Mkopo kwa mtu mwenye ulemavu

7.-(1) Bila kujali masharti ya kanuni ya 6, mtu mwenye ulemavu atakuwa na sifa ya kupata mkopo na kuchukuliwa kuwa ni kikundi cha watu wenye ulemavu endapo:

(a) timu ya menejimenti itajiridhisha kuwa mtu huyo amekosa mtu mwingine mwenye ulemavu na sifa ya kuwa mwanakikundi wa kikundi cha watu wenye ulemavu;

(b) anajishughulisha na ujasiriamali au anakusudia kuanzisha shughuli za ujasiriamali mdogo au wa kati;

(c) ana akaunti ya benki iliyofunguliwa kwa jina lake kwa shughuli maalum za kiujasiriamali; na

(d) hana ajira rasmi.

(2) Masharti mengine ya Kanuni hizi yatatumika kwa mtu mwenye ulemavu atakayepatiwa mkopo kwa mujibu wa masharti ya kanuni ya 6(1).

Utaratibu wa uombaji wa mikopo

8.-(1) Mamlaka ya Serikali za Mitaa itawajibika kutoa tangazo kwa umma kwa madhumuni ya kuutarifu umma na vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kuhusu kuwepo kwa fedha zilizotengwa kwa ajili ya mikopo ya vikundi.

(2) Kikundi kinachokusudia kuomba mkopo kitatuma maombi kwa Halmashauri kupitia mfumo wa kielektroniki wa utoaji na usimamizi wa mikopo.

(3) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (2), maombi ya mkopo yatazingatia utaratibu uliobainishwa katika mwongozo wa utoaji na usimamizi wa mikopo ya vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu katika mamlaka ya serikali za mitaa.

Utaratibu wa utoaji wa mikopo

9.-(1) Mamlaka ya Serikali za Mitaa itatakiwa kushughulikia maombi ya mikopo katika kipindi kisichozidi miezi miwili tangu tarehe ya mwisho ya kupokea maombi ya mkopo.

(2) Endapo maombi ya mkopo yamekubaliwa, Mamlaka ya Serikali za Mitaa itatakiwa kukitaarifu kikundi kilichokubaliwa kupata mkopo ndani ya muda wa siku saba tangu uamuzi wa kukubali maombi kufikiwa.

(3) Endapo maombi ya mkopo yatakataliwa, Mamlaka ya Serikali za Mitaa itatakiwa kukitaarifu kikundi kuhusu kukataliwa kwa maombi hayo pamoja na sababu zake ndani ya muda wa siku saba tangu uamuzi ulipofikiwa.

(4) Endapo maombi ya mkopo yataridhiwa, Mamlaka ya Serikali za Mitaa itatakiwa kuingiza kiasi cha mkopo kilichoridhiwa katika akaunti ya kikundi husika baada ya kusaini Mkataba na kikundi.

Matumizi ya fedha za mikopo

10.-(1) Fedha za mikopo zitakazotolewa chini ya Kanuni hizi zitatumika kwa miradi iliyoidhinishwa na Timu ya Menejimenti kwa kuzingatia ushauri na mapendekezo ya Kamati ya Huduma za Mikopo katika ngazi ya Halmashauri.

(2) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1), mkopo utakaotolewa chini ya Kanuni hizi unaweza kutekeleza mradi wa mwanakikundi mmoja mmoja na kikundi kitabaki kuwa dhamana ya mkopo.

(3) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1), kikundi kinaweza kubadilisha mradi baada ya kuomba na kupata idhini ya Timu ya Menejimenti.

Urejeshaji wa mikopo

11.-(1) Kikundi kilichopata mkopo chini ya Kanuni hizi kitatakiwa kuanza kurejesha mkopo baada ya miezi mitatu tangu siku ya kupata mkopo.

(2) Marejesho ya mkopo yatafanyika kila mwezi kwa kuzingatia viwango vilivyokubaliwa kati ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa na kikundi kilichopata mkopo.

(3) Bila kujali masharti ya kanuni ndogo ya (1) na (2), Mamlaka ya Serikali za Mitaa inaweza kuingia makubaliano na kikundi kilichopata mkopo kuhusu namna bora ya urejeshaji wa mkopo kulingana na aina ya mradi.

(4) Kikundi kilichopata mkopo kitawajibika kuwasilisha marejesho ya mkopo kupitia mfumo wa malipo ya serikali.

(5) Kikundi au mwanakikundi ataweka fedha zinazotokana na shughuli anayofanya iliyopatiwa mkopo kwenye akaunti ya benki iliyofunguliwa kila anapopokea mapato baada ya kutoa matumizi kwa ajili ya akiba na kulipa mkopo.

(6) Mamlaka ya Serikali za Mitaa zitakusanya au kufuatilia urejeshaji wa mikopo kutoka kwa vikundi kulingana na makubaliano yaliyoainishwa katika mkataba uliosainiwa kati ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa na kikundi.

Kuchelewesha marejesho ya mikopo

12.-(1) Mkopo wenye tarehe maalum ya rejesho utachukuliwa kuwa umecheleweshwa wote ikiwa sehemu ya rejesho au malipo yanayodaiwa kimkataba hayajalipwa.

(2) Mikopo inayorejeshwa kwa awamu itachukuliwa kuwa yote imecheleweshwa ikiwa awamu yoyote inayotakiwa kurejeshwa imecheleweshwa kwa siku moja au zaidi.

(3) Mkopo wa kikundi utachukuliwa kuwa wote umecheleweshwa pale ambapo mwanakikundi ameshindwa kurejesha na kiasi kinachotakiwa kurejeshwa hakijarejeshwa na wanakikundi.

(4) Endapo kikundi kitachelewesha marejesho kwa mujibu wa mkataba, Mamlaka ya Serikali za Mitaa itatoa notisi ya siku saba kukitaka kikundi kufanya marejesho.

(5) Endapo baada ya muda wa siku saba kikundi kitashindwa kafanya marejesho, Mamlaka ya Serikali za Mitaa itakiita kikundi kilichochelewesha marejesho kwa ajili ya ushauri na kuingia makubaliano ya namna ya kurejesha kiasi ambacho hakijalipwa.

Kushindwa kurejesha mkopo

13.-(1) Endapo kikundi kilichopata mkopo kitashindwa kurejesha mkopo kwa mujibu wa makubaliano, mkataba au muda uliopangwa chini ya kanuni ya 12(5), Mamlaka ya Serikali za Mitaa itakipa kikundi hicho notisi ya siku thelathini ya kukitaka kurejesha mkopo unaopaswa kulipwa.

(2) Endapo kikundi kitashindwa kurejesha mkopo baada ya muda wa nyongeza, Mamlaka ya Serikali za Mitaa itatoa notisi kwa kikundi hicho kuhusu kusudio la kufungua shauri mahakamani dhidi ya wanakikundi.

Nyongeza ya muda wa kurejesha mkopo

14. Bila kuathiri masharti ya muda wa kurejesha mkopo ulioainishwa kwenye Kanuni hizi, kikundi kilichopata mkopo kinaweza kuongezewa muda wa kurejesha mkopo huo kwa kuwasilisha maombi maalum kwa Mkurugenzi yakiainisha sababu za kushindwa kurejesha mkopo kwa wakati na mpango uliopo wa kurejesha mkopo katika muda wa nyongeza.

SEHEMU YA TATU
USIMAMIZI WA MIKOPO

Majukumu ya Mkurugenzi

15. Mkurugenzi wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa atakuwa na wajibu wa kutekeleza majukumu yafuatayo:

(a) kusimamia urejeshaji wa mikopo ya vikundi kwa wakati;

(b) kuwasilisha mapendekezo ya maombi ya mikopo ya vikundi kwenye kamati ya wilaya ya uhakiki wa mikopo;

(c) kuchukua hatua stahiki kwa vikundi vinavyokiuka masharti ya Kanuni hizi;

(d) kuwasilisha taarifa za utoaji na usimamizi

wa mikopo kwa kila robo katika ofisi ya Mkuu wa Mkoa;

(e) kusimamia utekelezaji wa taarifa za ukaguzi;

(f) kuwezesha na kusimamia utendaji kazi wa kamati za huduma za mikopo ya vikundi ngazi ya kata na halmashauri; na

(g) kuwezesha mafunzo kwa wasimamizi, kamati na vikundi.

Majukumu ya Afisa Maendeleo ya Jamii

16.-(1) Afisa Maendeleo ya Jamii wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa atakuwa na majukumu yafuatayo:

(a) kutambua vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu;

(b) kuratibu mikopo ya vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu;

(c) kupokea maombi ya mikopo yaliyowasilishwa na vikundi;

(d) kusimamia uhai na kulinda maslahi ya vikundi na kuvijengea uwezo katika kufanikisha shughuli za uchumi;

(e) kufuatilia marejesho ya mikopo;

(f) kuhakikisha mikopo inayotolewa inatumika kama ilivyokusudiwa;

(g) kuandaa na kuwasilisha taarifa ya mikopo iliyotolewa kwa Kamati ya Huduma za Mikopo;

(h) kuandaa taarifa ya kila robo mwaka na kuiwasilisha kwenye vikao vya kisheria vya Mamlaka ya Serikali ya Mitaa;

(i) kuwa kiungo kati ya vikundi na Kamati ya Huduma za Mikopo;

(j) kutunza kumbukumbu za mikataba, mikopo na marejesho ya vikundi vilivyopewa mikopo;

(k) kuhamasisha uanzishaji wa vikundi kwa kuzingatia fursa zilizopo katika maeneo husika; na

(l) kushirikiana na afisa biashara katika kuunganisha vikundi na taasisi zenye fursa

mbalimbali za kiuchumi.

(2) Katika kutekeleza majukumu yaliyoainishwa katika kanuni ndogo ya (1), Afisa Maendeleo ya Jamii atatakiwa kushirikiana na wataalamu wa sekta nyingine wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

Majukumu ya Afisa Biashara

17. Afisa Biashara wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa atakuwa na majukumu yafuatayo:

(a) kushirikiana na wajumbe wengine wa Kamati ya Huduma za Mikopo kuhakikisha vikundi vinavyoibuliwa vinawezeshwa kutumia fursa za kibiashara zilizopo ndani na nje ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa;

(b) kuunganisha vikundi na sekta mbalimbali za uzalishaji;

(c) kuviwezesha vikundi vinavyojihusisha na uzalishaji wa bidhaa kupata alama za ubora wa biashara;

(d) kushirikiana na Afisa Maendeleo ya Jamii katika kuunganisha vikundi na taasisi zenye fursa;

(e) kushirikiana na wataalamu wa sekta nyingine kutafuta masoko ya ndani na nje ya Halmashauri kwa bidhaa zinazozalishwa na vikundi; na

(f) kuhamasisha vikundi kujirasimisha kibiashara ili kuongeza wigo wa fursa ya soko la bidhaa wanazozalisha.

Wajibu wa Mweka Hazina

18. Mweka Hazina wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa atakuwa na wajibu wa kufanya malipo na kuhasibu fedha za mikopo ya vikundi.

Wajibu wa Mkaguzi wa Ndani

19. Mkaguzi wa Ndani wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa atakuwa na wajibu chini ya Kanuni hizi wa kukagua fedha zilizotengwa kwa ajili ya mikopo ya vikundi, miradi ya vikundi, urejeshaji na usimamizi wa mikopo kila robo mwaka.

Kamati ya huduma za

20. Kutakuwa na Kamati ya Huduma za Mikopo

mikopo ngazi ya kata

ngazi ya Kata katika kila Mamlaka ya Serikali za Mitaa itakayokuwa na wajumbe wafuatao:

(a) Mtendaji wa Kata ambaye atakuwa Mwenyekiti wa Kamati;
(b) Afisa Maendeleo ya Jamii Kata ambaye atakuwa Katibu wa Kamati;
(c) Afisa Ustawi wa Jamii Kata;
(d) Maafisa Ugani wa Kata;
(e) Afisa Elimu Kata;
(f) Polisi Kata; na
(g) Watendaji wa vijiji au mtaa.

Majukumu ya Kamati ya Huduma ya Mikopo ngazi ya Kata

21. Kamati ya Huduma ya Mikopo itakuwa na majukumu yafuatayo:

(a) kupokea, kujadili na kuchambua maombi ya mikopo yaliyopokelewa;
(b) kufanya tathmini ya awali ya maombi yaliyowasilishwa, kutembelea, kuhakiki na kushauri kuhusu vikundi vilivyoomba mikopo ;
(c) kuwasilisha taarifa ya maombi ya mikopo kwa Kamati ya Huduma za Mikopo ngazi ya Halmashauri;
(d) kufanya ufuatiliaji wa marejesho kwa vikundi vilivyopewa mikopo;
(e) kufanya ufuatiliaji wa vikundi kuona maendeleo ya shughuli zao;
(f) kushirikisha wadau kutoa mafunzo kwa vikundi; na
(g) kuwasilisha taarifa ya mikopo kwa Kamati ya Maendeleo ya Kata.

Kamati ya Huduma ya Mikopo ngazi ya Halmashauri

22.-(1) Kutakuwa na Kamati ya Huduma ya Mikopo ngazi ya Halmashauri katika kila Mamlaka ya Serikali za Mitaa itakayokuwa na wajumbe wafuatao:

(a) Mkuu wa Divisheni au Kitengo atakayeteuliwa na Mkurugenzi ambaye atakuwa Mwenyekiti wa Kamati;
(b) Mweka Hazina;
(c) Mkuu wa Divisheni ya Mipango na Uratibu;

(d) Afisa Ushirika;
(e) Afisa Ustawi wa Jamii;
(f) Mkuu wa Divisheni ya Maendeleo ya Jamii ambaye atakuwa Katibu wa Kamati.
(g) Mratibu wa Mikopo;
(h) Afisa Biashara; na
(i) Afisa Vijana.

(2) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1), Kamati inaweza kumwalika mtaalamu yeyote kuisaidia Kamati, isipokuwa mtu huyo hatakuwa na haki ya kupiga kura.

Majukumu ya Kamati ya Huduma ya Mikopo ngazi ya Halmashauri

23. Kamati ya Huduma ya Mikopo ngazi ya Halmshauri itakuwa na majukumuyafuatayo:
(a) kupokea na kujadili taarifa ya uchambuzi wa vikundi vilivyoomba mikopo kutoka katika kamati ya huduma ya mikopo ya kata;
(b) kufanya tathmini ya maombi yaliyowasilishwa na kutoa mapendekezo ya kutoa mikopo kwa vikundi na waombaji waliokidhi vigezo;
(c) kuandaa taarifa ya maombi ya vikundi na mapendekezo ya kupewa au kutopewa mikopo na kuwasilisha kwenye timu ya menejimenti ya halmashauri;
(d) kuhakikisha kuwa wanufaika wa mikopo wanapata taarifa kuhusu kufunguliwa kwa dirisha la mikopo kwa wakati;
(e) kuratibu mafunzo ya uendeshaji wa shughuli za kiuchumi, biashara na usimamizi wa fedha kwa vikundi;
(f) kufanya ufuatiliaji kwa vikundi vilivyopewa mikopo kuona shughuli zinazotekelezwa na kutoa ushauri wa kitaalamu pale inapohitajika;
(g) kufuatilia marejesho ya mikopo na kutoa ushauri katika eneo la urejeshaji na utunzaji wa kumbukumbu za mikopo;
(h) kuibua na kujadili fursa zilizopo ndani ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa ili ziweze kutumiwa katika kuhamasisha uanzishaji

wa vikundi kwa ajili ya kupata mikopo; na
(i) kutekeleza suala lolote linalohusu utekelezaji wa Kanuni hizi kwa kadri itakavyoelekezwa na Timu ya Menejimenti.

Kamati ya Wilaya ya Uhakiki wa Mikopo

24. Kutakuwa na Kamati ya Uhakiki kwa kila Mamlaka za Serikali za Mitaa ambayo itakuwa na wajumbe wafuatao:
(a) Katibu Tawala Wilaya ambaye atakuwa Mwenyekiti wa Kamati;
(b) mjumbe mmoja kutoka Ofisi ya Usalama ya Wilaya;
(c) mjumbe mmoja kutoka Ofisi ya TAKUKURU Wilaya;
(d) mjumbe mmoja kutoka Kamati ya Uratibu wa Mikopo ngazi ya Mkoa; na
(e) Mkuu wa Divisheni ya Maendeleo ya Jamii wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa ambaye atakuwa Katibu wa Kamati.

Majukumu ya Kamati ya Wilaya ya Uhakiki wa Mikopo

25. Kamati ya uhakiki itakuwa na majukumu yafuatayo:
(a) kupokea na kujadili taarifa ya mapendekezo ya vikundi vilivyowasilisha maombi ya mkopo kutoka timu ya menejimenti; na
(b) kutoa ushauri kwa timu ya menejimenti kuhusu vikundi vilivyopendekezwa kupewa mkopo.

Majukumu ya Timu ya Menejimenti

26. Katika kushughulikia maombi ya mikopo inayotolewa chini ya Kanuni hizi, Timu ya Menejimenti itakuwa na majukumu yafuatayo:
(a) kupokea na kujadili mapendekezo ya mikopo kutoka Kamati ya Huduma ya Mikopo ya Halmashauri;
(b) kuwasilisha orodha ya vikundi vilivyopendekezwa kupewa mikopo kwa Kamati ya Wilaya ya Uhakiki wa Mikopo;
(c) kupokea taarifa ya uhakiki wa mikopo kutoka Kamati ya Wilaya ya Uhakiki wa Mikopo;
(d) kuidhinisha mikopo kwa vikundi

vilivyokidhi vigezo baada ya kuhakikiwa na kamati ya wilaya ya uhakiki;

(e) kufuatilia marejesho ya mikopo;

(f) kupokea taarifa za hali ya utoaji na urejeshaji wa mikopo kutoka Kamati ya Huduma ya Mikopo ya Halmashauri;

(g) kuwasilisha orodha ya vikundi vilivyopendekezwa kupewa mikopo kwa Kamati ya Wilaya ya Uhakiki wa Mikopo;

(h) kujadili na kuwasilisha taarifa ya robo mwaka ya utekelezaji wa Kanuni hizi katika ofisi ya Mkuu wa Mkoa.

Majukumu ya Kamati ya Kudumu ya Fedha, Uongozi na Mipango na kamati ya kudumu ya fedha na utawala

27. Kamati ya Kudumu ya Fedha, Uongozi na Mipango katika mamlaka ya wilaya na Kamati ya Kudumu ya Fedha na utawala katika mamlaka za miji zitakuwa majukumu yafuatayo:

(a) kupokea taarifa ya fedha zilizotengwa na kutolewa kwenye vikundi;

(b) kukagua miradi ya vikundi vilivyopata mikopo kwa kufuata utaratibu wa kawaida wa ukaguzi wa miradi ndani ya eneo la Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

Majukumu ya Baraza la Madiwani

28. Baraza la Madiwani litakuwa na jukumu la kupokea taarifa ya mikopo.

Wajibu wa Kamati ya Bajeti ya Halmashauri

29. Kutakuwa na Kamati ya Bajeti ya Halmashauri itakayokuwa na majukumu yafuatayo:

(a) kutenga bajeti ya asilimia kumi ya mapato ya ndani yasiyolindwa kwa ajili ya mikopo ya vikundi;

(b) kutenga fedha ya asilimia kumi ya mapato ya ndani ya yasiyolindwa kwa ajili ya mikopo ya vikundi; na

(c) kutathmini utekelezaji wa bajeti ya asilimia kumi.

Kamati ya uratibu wa Mikopo ngazi ya Mkoa

30. Kutakuwa na Kamati ya Uratibu wa Mikopo ngazi ya Mkoa itakayokuwa na wajumbe wafuatao:

(a) Mkuu wa Sehemu au Kitengo ambaye

atateuliwa na Katibu Tawala wa Mkoa na atakuwa Mwenyekiti wa Kamati;

(b) Katibu tawala msaidizi sehemu ya mipango na uratibu ambaye atakuwa Katibu wa Kamati;

(c) Katibu tawala msaidizi sehemu ya menejimenti, ufuatiliaji na ukaguzi;

(d) Afisa Maendeleo ya Jamii anayeratibu mikopo;

(e) Afisa kutoka sehemu ya uchumi na uzalishaji;

(f) Afisa kutoka sehemu ya viwanda, biashara na uwekezaji;

(g) Afisa Ustawi wa Jamii; na

(h) Afisa Usimamizi wa Fedha.

Majukumu ya kamati ya uratibu wa mikopo ngazi ya mkoa

31. Kamati ya uratibu wa mikopo ngazi ya mkoa itakuwa na majukumu yafuatayo:

(a) kuhakikisha Mamlaka ya Serikali za Mitaa zinatenga asilimia kumi ya mapato ya ndani kwa ajili ya mikopo kwa vikundi;

(b) kusimamia utoaji wa mafunzo katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa;

(c) kuchambua na kuandaa taarifa ya utoaji, usimamizi na urejeshaji wa mikopo ngazi ya mkoa;

(d) kutoa taarifa ya utoaji na urejeshaji wa mikopo kwa Katibu Tawala wa Mkoa;

(e) kumshauri Katibu Tawala wa Mkoa kuchukua hatua stahiki kwa halmashauri zisizozingatia sheria, kanuni na taratibu za mikopo;

(f) kuhakikisha kuwa halmashauri zinasimamia uundaji wa vikundi kulingana na fursa za kiuchumi zilizopo katika maeneo yao;

(g) kumshauri Katibu Tawala wa Mkoa kufanya kikao cha tathmini kabla na baada ya utekelezaji wa utoaji na urejeshaji wa mikopo pamoja na shughuli za vikundi pale inapohitajika na kuwasilisha taarifa kwa Wizara;

(h) kufuatilia utekelezaji wa miradi ya vikundi vilivyoanzishwa kutokana na mikopo ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, kubaini mafanikio na changamoto na kutoa ushauri; na

(i) kutekeleza majukumu mengine yanayohusu utoaji, usimamizi na urejeshaji wa mikopo.

Kitengo cha uratibu wa utoaji na usimamizi wa mikopo ya vikundi

32.-(1) Katika kusimamia utekelezaji wa Kanuni hizi, kutakuwa na Kitengo cha Uratibu wa Utoaji na Usimamizi wa Mikopo ya Vikundi katika Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

(2) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1), Kitengo cha Uratibu wa Utoaji na Usimamizi wa Mikopo ya Vikundi kitakuwa na majukumu yafuatayo:

(a) kuandaa na kusimamia mifumo ya uendeshaji na utoaji wa mikopo ya vikundi ;

(b) kusimamia utekelezaji wa makubaliano ya Serikali na Taasisi za Fedha kuhusu utoaji, usimamizi na urejeshaji wa mikopo;

(c) kufanya ufuatiliaji na kuhakikisha Ofisi za Wakuu wa Mikoa zinatekeleza majukumu ya uratibu na usimamizi wa shughuli za mikopo;

(d) kupokea taarifa, kuzichambua na kushauri juu ya utekelezaji wa utoaji na urejeshaji wa mikopo;

(e) kufanya ufuatiliaji shirikishi wa utengaji, utoaji na urejeshaji wa mikopo kwa mujibu wa kanuni hizi;

(f) kuandaa na kufanya mapitio ya sheria, kanuni na miongozo inayohusu utoaji na urejeshaji wa mikopo;

(g) kujenga uwezo wa wasimamizi wa mikopo katika ngazi za mikoa na halmashauri;

(h) kuhakikisha mamlaka za serikali za mitaa zinatenga fedha za mikopo kwa mujibu wa Sheria;

(i) kuratibu vikao vya tathmini ya utoaji na urejeshaji wa mikopo kwa kadri itakavyohitajika;

(j) kutekeleza majukumu mengine yanayohusiana na mikopo kwa vikundi;
(k) kufanya utafiti na uchambuzi wa shughuli za utoaji wa mikopo ya vikundi; na
(l) kushauri masuala ya kisera kuhusu shughuli za utoaji wa mikopo ya vikundi.

SEHEMU YA NNE
UTOAJI WA MIKOPO KWA UTARATIBU WA TAASISI ZA FEDHA

Utoaji wa Mikopo kwa utaratibu wa taasisi za fedha

33.-(1) Mamlaka ya Serikali za Mitaa inaweza kutoa mikopo kwa utaratibu wa kutumia taasisi za fedha.

(2) Endapo Mamlaka ya Serikali za Mitaa itatumia utaratibu wa kutoa mikopo wa kutumia taasisi za fedha, itatakiwa kuingia makubaliano ya kimkataba na taasisi za fedha kabla ya kuanza mchakato wa utoaji wa mikopo.

(3) Mkataba utabainisha masharti na vigezo vya utoaji wa mikopo, majukumu na haki za pande zote, na utaratibu wa utekelezaji na usimamizi wa mikopo hiyo.

(4) Taasisi ya fedha itatoa mikopo baada ya kufanya uchambuzi wa vikundi vilivyowasilishwa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

Ufuatiliaji na Ukusanyaji wa Marejesho

34.-(1) Taasisi za fedha zitakuwa na jukumu la msingi la kufuatilia na kukusanya marejesho kwa mujibu wa masharti yaliyoainishwa katika mkataba uliosainiwa kati ya taasisi za fedha na kikundi husika ambacho kimepokea mkopo.

(2) Kila kikundi husika kinachopokea mkopo kitawajibika kurejesha mkopo kwa wakati na kwa kiwango kilichokubaliwa kama ilivyoainishwa katika mkataba.

(3) Utaratibu wa ukusanyaji wa marejesho utabainishwa katika mkataba, ukiwa na vipengele vya kushughulikia ucheleweshaji na kutokurejesha mikopo.

Majukumu ya pande zote

35.-(1) Mamlaka ya Serikali za Mitaa na taasisi za fedha zinapaswa kushirikiana kwa karibu katika utekelezaji wa utoaji wa mikopo.

(2) Mamlaka ya Serikali za Mitaa itakuwa na jukumu la kutoa ushirikiano kwa taasisi za fedha katika ufuatiliaji wa mikopo.

(3) Taasisi za fedha zinapaswa kutoa taarifa za mara kwa mara kwa Mamlaka ya Serikali za Mitaa kuhusu hali ya mikopo iliyotolewa, ikijumuisha taarifa za marejesho na changamoto zinazojitokeza.

Tathmini na uboreshaji

36.-(1) Mamlaka ya Serikali za Mitaa na taasisi za fedha zitafanya tathmini ya mara kwa mara ya utekelezaji wa utoaji wa mikopo kubaini mafanikio na changamoto zinazojitokeza.

(2) Mapendekezo ya maboresho yatapaswa kuzingatiwa na kutekelezwa kwa wakati kuhakikisha ufanisi na tija katika utoaji wa mikopo.

SEHEMU YA TANO
MASHARTI YA JUMLA

Akaunti Maalum ya Mikopo

37.-(1) Kwa kuzingatia sheria na taratibu za usimamizi wa fedha za umma, kila Mamlaka ya Serikali za Mitaa itatakiwa kufungua na kuendesha Akaunti Maalum ya Mikopo itakayofunguliwa katika mojawapo ya benki zinazotoa huduma katika eneo la Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

(2) Mkurugenzi atakuwa na wajibu wa kuhakikisha kuwa fedha zote zilizotengwa kwa ajili ya mikopo inayotolewa chini ya Kanuni hizi na fedha za marejesho ya mikopo hiyo zinahifadhiwa katika Akaunti Maalum ya Mikopo.

Mafunzo na ufuatiliaji wa mikopo ya vikundi

38.-(1) Mamlaka ya serikali za mitaa itakuwa na wajibu wa-

(a) kutoa mafunzo kwa vikundi vinavyotarajiwa na vilivyokubaliwa kupata mkopo ikiwemo masuala ya uwekaji wa akiba, uundaji wa vikundi vyenye tija, uongozi, usimamizi wa fedha, uendeshaji wa miradi na utoaji wa taarifa hususan zinazohusu miradi inayotekelezwa na mkopo husika; na

(b) kufanya ufuatiliaji wa mikopo na tathmini ya maendeleo ya vikundi vilivyopata mikopo.

(2) Kwa madhumuni ya utekelezaji wa masharti ya kanuni ndogo ya (1), mamlaka ya serikali za mitaa itatenga fedha kutoka katika fedha za mikopo kwa uwiano ufuatao:

(a) halmashauri inayochangia asilimia 70 ya mapato ya ndani kwenye miradi ya maendeleo itatenga asilimia 5 ya fedha zinazotarajiwa kutolewa kwa ajili ya mikopo kwa mwaka husika;

(b) halmashauri inayochangia asilimia 60 ya mapato ya ndani kwenye miradi ya maendeleo itatenga asilimia 10 ya fedha zinazotarajiwa kutolewa kwa ajili ya mikopo kwa mwaka husika;

(c) halmashauri inayochangia asilimia 40 ya mapato ya ndani kwenye miradi ya maendeleo itatenga asilimia 15 ya fedha zinazotarajiwa kutolewa kwa ajili ya mikopo kwa mwaka husika; na

(d) halmashauri inayochangia asilimia 20 ya mapato ya ndani kwenye miradi ya maendeleo itatenga asilimia 20 ya fedha zinazotarajiwa kutolewa kwa ajili ya mikopo kwa mwaka husika.

Kuhitimu ukopaji

39.-(1) Kwa mujibu wa anuni hizi vikundi vitafikia hatua ya kuhitimu kunufaika na mikopo, baada ya taarifa ya tathmini kubaini uwezo wa kikundi kujisimamia na kujiendesha kibiashara.

(2) Taratibu za kuhitimisha vikundi zitafafanuliwa kwenye mwongozo wa utoaji na usimamizi wa mikopo.

Makosa na adhabu

40.-(1) Kikundi au mtu yeyote-

(a) atakayetumia fedha za mkopo uliotolewa chini ya Kanuni hizi kwa matumizi ambayo hayakuidhinishwa na Timu ya Menejimenti; au

(b) atakayetoa taarifa za uongo kwa lengo la kupata mkopo unaotolewa chini ya Kanuni hizi,

(c) atakuwa ametenda kosa na endapo atatiwa hatiani atawajibika kulipa faini ya kiasi kisichopungua shilingi laki mbili na kisichozidi shilingi milioni moja au kutumikia kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne.

(2) Bila kuathiri kanuni ndogo ya (1), kikundi kitakachopatikana na hatia kwa kosa chini ya kanuni ndogo ya (1) kitapaswa kurejesha fedha sawa na kiwango kilichopokea.

Kufutwa kwa Kanuni TS Na.

41.-(1) Kanuni za Utoaji na Usimamizi wa Mikopo kwa Vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu za mwaka 2019 zinafutwa.

286 la 2019

(2) Bila kuathiri kanuni ndogo ya (1), mikopo iliyotolewa kabla ya Kanuni hizi itasimamiwa kwa utaratibu wa marejesho ulioainishwa katika Kanuni hizi.

Dodoma,
2 Oktoba, 2024

MOHAMED O. MCHENGERWA,
Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais,
Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa